LEGAL AND HUMAN RIGHTS CENTRE

LHRC

KITUO CHA SHERIA NA HAKI ZA BINADAMU



# MCHAKATO WA KATIBA MPYA
## NINI MWISHO WAKE?

*Kwa Jamii Yenye Haki na Usawa*

**Kimetayarishwa na;**

Bw. William Kahale na Bi. Fortunata Ntwale

**Kimehaririwa na:**

Dkt. Helen Kijo-Bisimba

Adv. Anna Henga

Adv. Naemy Sillayo

Paul Mikongoti

Felister Mauya

Fundikila Wazambi

Michael Mallya

**Kimechapishwa na:**

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC)

©

**LHRC**

Mei 2018

# YALIYOMO


YALIYOMO ii
SHUKRANI iii
UTAMBULISHO WA KITUO iii
MAONO iii
TAMKO LA LENGO MAHSUSI iii
LENGO KUU iii
DIBAJI iv
UTANGULIZI v

**SEHEMU YA KWANZA 1**
SABABU ZA KUKWAMA KWA MCHAKATO WA KATIBA 1

**SEHEMU YA PILI 3**
SHERIA ZA MCHAKATO WA MABADILIKO YA KATIBA 3

**SEHEMU YA TATU 4**
NJIA ZINAZOPENDEKEZWA KUKWAMUA MCHAKATO WA KATIBA 4
3.1. Kuitishwa kwa Kura ya Maoni na Kuzinduliwa Katiba Mpya; 4
3.1.1 Faida za Njia hii; 5
3.1.2 Mapungufu ya Njia Hii; 6
3.2 Kuitisha Bunge Maalum la Katiba; 6
3.2.1 Faida za Njia hii; 6
3.2.2 Mapungufu ya Njia hii; 6
3.3 Kuundwa kwa Kamati ya Wataalam wa Katiba; 7
3.3.1 Faida za Kuunda Kamati ya Wataalam; 9
3.3.2 Mapungufu ya Kuunda Kamati ya Wataalam; 9

**SEHEMU YA NNE 10**
HITIMISHO 10

# SHUKRANI

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kinapenda kutoa shukrani kwa Timu ya Wataalam iliyofanya uchambuzi na kuandaa ripoti kubwa ya Mkwamo wa Katiba Tanzania ambayo ndiyo iliyochagiza kuandikwa kwa kijitabu hiki kidogo. Kijitabu hiki kinalenga kutoa elimu juu ya Mkwamo wa Mchakato wa Katiba kwa umma. Pia shukrani za dhati zinatolewa kwa wafanyakazi wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu Bw. William B. Kahale na Bi. Fortunata Ntwale kwa kuandaa kijitabu hiki na Bodi ya Uhariri ya Kituo kwa uhariri.

# UTAMBULISHO WA KITUO

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC) ni shirika binafsi, huru, la kujitolea na la hiyari ambalo si la kisiasa wala kibiashara. Kituo kimeandikishwa na kusajiliwa kwa mujibu wa sheria za Tanzania mnamo Septemba 1995. Kabla ya kusajiliwa kama chombo huru, Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kilikuwa ni mradi wa haki za binadamu wa Mfuko wa Kuendeleza Elimu ya Sheria Tanzania (TANLET). Makao makuu ya Kituo yapo Dar es salaam wakati ambapo Arusha kuna Ofisi ndogo.

# MAONO

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kina taamali jamii yenye haki na usawa.

# TAMKO LA LENGO MAHSUSI

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu ni shirika lisilo la kiserikali wala kibiashara linalojibidiisha kukuza uwezo wa jamii ili kukuza, kuendeleza na kulinda haki za binadamu na utawala bora nchini.

# LENGO KUU

Lengo kuu la Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu ni kukuza uelewa wa sheria na haki za binadamu kwa jamii kwa ujumla na hasa wale wanajamii ambao kwa sababu moja au nyingine wameachwa nyuma. Uelewa unakuzwa kwa njia ya elimu na msaaada wa Sheria.

# DIBAJI

Ni takribani miaka 23 tangu kuanzishwa kwa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu. Katika kipindi hicho chote Kituo kimekua kikiendesha programu mbalimbali za elimu ya Haki za Binadamu ikiwemo kupigania kuwepo kwa Katiba Mpya ya nchi inayoakisi maoni ya wananchi.

Tanzania iliamua kuanza uandishi wa katiba mpya kutokana na kua katiba zote tano zilizopita tangu katiba ya uhuru ya mwaka 1961 mpaka katiba ya kudumu ya mwaka 1977 pamoja na marekebisho yake yote 14 vimekuwa vikilalamikiwa kwa kutoshirikisha wananchi kikamilifu. Hivyo ukaundwa mfumo ambao ungeruhusu ushiriki wa wananchi katika kupata katiba bora.

Pamoja na kukwama kwa  kwa mchakato wa mabadiliko ya katiba mnamo mwezi Aprili 2015 ambao ulianzishwa mnamo mwaka 2011 , bado Kituo kinaamini kuwa kuna umuhimu mkubwa na wa haraka wa kuendeleza mchakato huo kutokana na sababu mbalimbali.Kwa kutambua umuhimu huo, Kituo kimeona umuhimu wa kuandaa kitabu hiki kidogo ambacho ni zao la ripoti ya uchambuzi mkubwa wa kina uliofanywa na wataalam wa masuala ya Katiba na Sheria kutoka chuo kikuu cha Dar es Salaam.

Kitabu hiki kinaweka bayana mambo makuu mawili ambayo ni sababu kuu za kukwama kwa mchakato wa katiba; na mapendekezo ya njia nzuri za kuufufua na kuendeleza mchakato wa Katiba ambao unabeba maoni ya wananchi.

Ni matumaini yangu kwamba kitabu hiki kitachangia kukuza uelewa wa wananchi juu ya sababu za mkwamo wa mchakato wa Katiba na njia ambazo zinapendekezwa kuchukuliwa katika kuendeleza mchakato wa Mabadiliko ya Katiba kwa kuzingatia maoni ya wananchi.

**Dkt. Helen Kijo - Bisimba**

**Mkurugenzi Mtendaji**

# UTANGULIZI

Tarahe 31 Disemba 2010 aliyekuwa Rais wa awamu ya nne wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dk. Jakaya Mrisho Kikwete alitangaza nia ya Serikali ya kuanzisha mchakato wa Katiba. Hatimaye mwaka 2011 Mchakato huo ulianza kwa kutungwa kwa Sheria ya Mabadiliko ya Katiba Na. 83/2011 na baadaye kufuatiwa na Sheria nyingine ya Kura ya Maoni Na. 11/2013.

Sheria ya Mabadiliko ya Katiba ilitamka kuanzishwa kwa Tume ya Mabadiliko ya Katiba ambayo iliratibu mchakato wa kukusanya maoni ya wananchi na kuandaa rasimu ya kwanza ya katiba ambayo pia ilihaririwa na Mabaraza ya Katiba na hatimaye kupatikana kwa Rasimu ya Pili ya Katiba. Rasimu hiyo iliwasilishwa kwenye Bunge Maalum la Katiba (BMK) ambalo kwa kiasi kikubwa lilitawaliwa na wanasiasa wakitokana na wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na wajumbe wa Baraza la Wawakilishi -Zanzibar.

Mchakato wa Bunge Maalum kujadili na kutunga Katiba Inayopendekezwa kwa kiasi kikubwa ulitawaliwa na mivutano ya kisiasa na kusababisha baadhi ya wajumbe wa Bunge Maalum la Katiba kujitoa kwenye majadiliano na kuunda Umoja wa Katiba ya Wananchi (UKAWA). Kujitoa kwa wajumbe hawa kulisababisha kutungwa kwa Katiba Inayopendekezwa iliokosa muafaka na kuidhinishwa Mwezi Oktoba 2014.

Kwa mujibu wa Sheria ya Kura ya Maoni Na. 11/2013, Tume ya Uchaguzi ilipanga tarehe 30 Aprili 2015 kuwa ndiyo siku ya wananchi kupiga kura ya maoni. Zoezi la kura ya maoni lilikwama kufanyika kwa sababu mbalimbali ambazo zinabainishwa katika kitabu hiki. Tangu kipindi hicho hadi sasa pamekuwa na kukwama kuendelea kwa mchakato ulioanza kwa Nguvu na uliowaamsha wananchi wengi kuitaka Katiba mpya ya nchi. Uwepo wa Serikali mpya ya awamu ya tano pia haukusaidia sana kwani Rais wa awamu hii ametamka wazi kuwa hiki si kipaumbele cha serikali yake. Kwa jinsi zoezi hili lilipokuwa limefikia na gharama ambazo tayari zimetumika za fedha na hata muda na ari za watu ipo haja ya kuangalia nini kinachoweza kufanyika kututoa hapa.

## SABABU ZA KUKWAMA KWA MCHAKATO WA KATIBA

Kwa mujibu wa Sheria ya Kura ya Maoni na Maelekezo ya Tume ya Uchaguzi (NEC), zoezi la kura ya maoni lilipangwa kufanyika tarehe 30 Aprili 2015. Lakini kutokana na sababu mbalimbali zoezi la kupiga kura ya maoni lilishindikana na kuahirishwa kwa kipindi kisichofahamika.

Sababu mbalimbali zilizopelekea kuahirishwa kwa zoezi la upigaji wa kura ya maoni juu ya Katiba Inayopendekezwa ni pamoja na;

i. Kutengwa kwa muda finyu na usio halisi wa kisheria kutekeleza zoezi la Upigaji kura ya Maoni. Kwa mujibu wa Sheria ya Kura ya Maoni, Rais aliiagiza Tume ya Uchaguzi kuandaa kura ya maoni kufanyika tarehe 30 Aprili 2015, lakini wakati huo huo Tume ya Uchaguzi ilikua ikiendesha programu ya kuboresha Daftari la Kudumu la Wapiga Kura kwa njia ya kielektroniki ili kutumika katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015. Kinyume na ilivyokua imepangwa, zoezi la kuboresha daftari lilichelewa kumalizika kwa muda muafaka, hivyo kupelekea muda kuwa finyu na hatimaye tarehe za kura ya maoni zilizopangwa kisheria kupitwa na wakati.

ii. Sababu nyingine ni kutokuwepo kwa muafaka wa kikatiba ndani ya Bunge Maalum la Katiba na hivyo kupelekea baadhi ya wajumbe wa BMK hususan waliotokana na Vyama vya Upinzani - Umoja wa Katiba ya Wananchi (UKAWA) kijitoa na kutoshiriki katika kuipitisha Katiba Inayopendekezwa na kuchangia kujitokeza kwa mgawanyiko mkubwa katika jamii na kuathiri mwenendo mzima wa mchakato wa katiba. Kwa kiasi kikubwa mpasuko wa BMK ulichangiwa na uwepo wa idadi kubwa ya wanasiasa ambao waliteuliwa kuwa wajumbe huku wakiwa bado ni wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na wajumbe wa Baraza la Wawakilishi -Zanzibar.

iii. Ujio wa awamu ya Tano ya Serikali, umeonyesha kutokuwepo kwa uwazi na nia ya dhati ya kuendeleza Mchakato wa Mabadiliko ya Katiba. Hii inadhihirishwa na kauli za mara kwa mara za viongozi mbalimbali wa serikali wakieleza kwamba Mchakato wa katiba sio kipaumbele cha Serikali ya awamu ya tano kinyume na madai makubwa ya makundi mbalimbali ya jamii ikiwemo Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kama mdau mmojawapo kuitaka serikali kuendeleza mchakato huo. Kauli hizi pia ni kinyume na Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2015, ambayo imeainisha wazi juu ya kukamilishwa kwa mchakato wa upatikanaji wa Katiba Mpya.

## SHERIA ZA MCHAKATO WA MABADILIKO YA KATIBA

Kama ilivyoelezwa awali, kuna sheria kuu mbili zilizoongoza mchakato wa mabadiliko ya katiba ambazo ni Sheria ya Mabadiliko ya Katiba Na. 83 ya mwaka 2011 pamoja na Sheria ya Kura ya Maoni Na. 11 ya mwaka 2013.

Sheria ya Mabadiliko ya katiba ilitoa muongozo wa kuundwa na mamlaka ya vyombo vyote vya kuratibu mchakato wa katiba, vikiwemo; Tume ya Mabadiliko ya Katiba, Mabaraza ya Katiba na Bunge Maalum la Katiba. Sharia hizi pia zimeainisha namna ya ushiriki wa wananchi katika hatua zote za mchakato wa katiba, utaratibu wa wananchi kuipigia kura ya Maoni Katiba Inayopendekezwa pamoja na vyombo vitakavyosimamia haswa Tume ya Taifa Uchaguzi.

Kwa kiasi kikubwa hatua zote za mchakato zinazotamkwa na Sheria ya Mabadiliko ya Katiba zimekwisha kamilika. Kwa upande wa Sheria ya Kura Maoni, hatua pekee ambayo haijakamilika mpaka sasa ni kupitishwa kwa Katiba Inayopendekezwa kupitia kura ya maoni na kuanza kutumika rasmi.

Wakati wa kutungwa kwa Sheria ya Kura ya Maoni, ilizaniwa kuwa mchakato wa katiba utakamilika ndani ya muda uliokuwa umekusudiwa kisheria. Kwa bahati mbaya muda ulikwisha kabla ya Katiba Inayopendekezwa kupigiwa kura ya maoni kutokana na sababu mbalimbali zilizoanishwa awali, ikiwemo uwepo wa zoezi la uandikishaji wa wapiga kura kwa njia ya kielektroniki kwa ajili ya uchaguzi mkuu wa mwaka 2015.

Kutokana na kupita kwa muda kisheria, maboresho ya Sheria ya Kura ya Maoni hayaepukiki ili kuruhusu mwendelezo mzima wa mchakato wa kupata katiba mpya.

# NJIA ZINAZOPENDEKEZWA KUKWAMUA MCHAKATO WA KATIBA

Kuna njia tatu zinazopendekezwa na Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu ambazo kituo kinadhani kwamba zingeweza kufanikisha kuufufua na kuuendeleza mchakato wa mabadiliko ya katiba kutokea ulipokomea. Njia hizi zitahitaji kutanguliwa na kujenga muafaka wa kikatiba kwa kuweka mazingira ya wananchi na makundi mbalimbali ya kijamii kujadiliana juu ya mchakato wa katiba pamoja na maboresho ya sheria zinazoongoza mchakato wa katiba, yaani Sheria Na. 83/2011 na 11/2013 ili kutoa nguvu ya kisheria kwa mwendelezo wa mchakato huo.

Njia tatu zinazopendekezwa ni pamoja na;

I. Kuitishwa kwa kura ya maoni na kuzinduliwa kwa Katiba Mpya
II. Kuitisha upya Bunge Maalum la Katiba ambalo ndilo lilitunga Katiba Inayopendekezwa
III. Kuteuliwa kwa Kamati Maalum ya Wataalam wa Masuala ya Sheria na Katiba. Njia hizi zinafafanuliwa kwa ufupi kama ifuatavyo

## 3.1. Kuitishwa kwa Kura ya Maoni na Kuzinduliwa Katiba Mpya;

Endapo hatua hii itaonekana kufaa, ni vema kuzingatia kwamba hatua pekee iliyosalia katika kuhitimisha mchakato wa katiba ni wananchi kupiga kura ya maoni juu ya Katiba Inayopendekezwa na kuzinduliwa kwa Katiba mpya kwa mujibu wa Sheria ya Kura ya Maoni. Lakini kutokana na kupitwa na wakati kwa baadhi ya vifungu vya sheria hii, inashauriwa kwamba maboresho ya msingi juu ya sheria hii yafanyike ili kuleta uhalali wa kisheria. Maboresho yanayopendekezwa yanajadiliwa hapa kwa ufupi:

ii. Inapendekezwa kwamba kifungu cha 4 cha Sheria ya Kura ya Maoni kiboreshwe kupitia mabadiliko madogo ya sheria ili kumpa mamlaka Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kushauriana na Rais wa Zanzibar kuiagiza Tume ya Taifa ya Uchaguzi kuendesha kura ya maoni juu ya Katiba Inayopendekezwa.

Pia kifungu kitamke kwamba tume iainishe kusudio la kupigwa kura ya maoni juu ya Katiba Inayopendekezwa, muda na tarehe za kupigwa kura ya maoni na kuainishwa mahsusi kwa swali litakaloulizwa kwa wananchi juu ya ama kuikubali au kuikataa Katiba Inayopendekezwa.

iii. Inapendekezwa kwamba kifungu cha 5 cha Sheria ya Kura ya Maoni kitoe mamlaka kwa Tume ya Taifa ya Uchaguzi kwamba ndani ya siku 14 ichapishe Notisi kwenye Gazeti la Serikali kuhusu swali litakaloulizwa kwa Wananchi juu ya Katiba Inayopendekezwa. Pia Tume iainishe muda wa kipindi cha Elimu ya Mpiga Kura na Kampeni ya kura ya maoni, muda na siku ya kupiga kura ya maoni. Pia inashauriwa kwamba kifungu cha 5(2) kifutwe kwa kupitwa na muda.

iv. Inapendekezwa kwamba Kifungu cha 34 (2) cha Sheria ya Kura ya Maoni kifanyiwe mabadiliko kwa mujibu wa hukumu ya Mahakama Kuu ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania katika shauri ***Na. 30 la mwaka 2015 kati ya Rashid Salum Adiy dhidi ya Waziri wa Katiba pamoja na Mwanasheria Mkuu wa Tanzania,*** ambapo Mahakama Kuu iliamuru kwamba; kifungu hiki kinakiuka masharti ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na hivyo Bunge likibadilishe na kusomeka katika kifungu 34(2) (b), ***'kura za Wazanzibari zilizoandikishwa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi'.***

### 3.1.1. Faida za Njia hii;

Endapo njia hii itachaguliwa kuendesha mchakato huu wa Katiba kuna faida mbili ambazo zinaonekana wazi nazo ni; kwanza ni kuonekana kukubalika kwa madai ya msingi ya wananchi na kurudisha imani kwa wananchi juu ya mchakato wa Katiba na nia nzuri ya serikali. Pamoja na uzuri wa njia hii, lakini ni vema wadau mbalimbali wakashirikishwa ili kujenga muafaka. Faida ya pili ya njia hii ni kujenga mazingira rafiki ya kikatiba ya uendeshaji wa zoezi la chaguzi za viongozi ikiwemo uchaguzi mkuu pamoja na chaguzi nyingine ndogo. Hii ni kwa kuzingatia kwamba kumekuwepo na madai ya msingi ya mara kwa mara kwa wadau wa uchaguzi kutoridhishwa na utendaji na uhuru wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi, malalamiko haya yaliweza kujibiwa kwa kiasi kikubwa katika Katiba Inayopendekezwa.

### 3.1.2. Mapungufu ya Njia Hii;

Mapungufu ya msingi ya njia hii endapo itafuatwa ni kuendelea kwa madai ya mabadiliko ya katiba hata baada ya kupitishwa kwa Katiba Inayopendekezwa. Hii ni kutokana na namna ambavyo Katiba Inayopendekezwa ilipitishwa ikiwa imekosa muafaka katika ngazi ya Bunge Maalum la Katiba baada ya kundi kubwa la wajumbe kutoka Umoja wa Katiba ya Wananchi (UKAWA) kususia vikao vya Bunge Maalum.

## 3.2. Kuitisha Bunge Maalum la Katiba;

Njia ya pili inayopendekezwa kufuatwa kuendeleza mchakato wa katiba ni kuitisha Bunge Maalum la Katiba kwa mara ya pili kuja kufanya maboresho muhimu ya Katiba Inayopendekezwa kwa mujibu wa kifungu cha 28 cha Sheria ya Mabadiliko ya Katiba Na. 83/2011 ambacho kinampa Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania mamlaka ya kufanya hivyo.

### 3.2.1. Faida za Njia hii;

Njia hii ni nzuri zaidi pengine kuliko njia nyingine mbili zinazopendekezwa katika kitabu hiki. Hii ni kwa sababu endapo Bunge Maalum la Katiba litaitishwa upya utapatikana upenyo wa mjadala wa wajumbe kwa kuzingatia makundi ya vyama vya siasa, kiraia na kijamii kujenga muafaka wa kikatiba na kufanyia marekebisho makubwa na ya msingi Katiba Inayopendekezwa kwa kuzingatia matakwa ya wananchi. Majadiliano ya kutosha katika Mchakato wa Katiba yatasaidia kujenga utamaduni wa kukubaliana na uvumilivu wa kisiasa katika jamii.

Ikumbukwe kwamba kanuni muhimu katika Mchakato wowote wa katiba ni kuwepo kwa uhuru wa wananchi kushiriki, kuafikiana na kumiliki mchakato wa kuandika katiba. Katiba inapaswa kutokana na muafaka. Na kwa sababu hii njia hii ikitumika Bunge maalum la Katiba itabidi liundwe upya kama ilivyoshawahi kupendekezwa. Liwe Bunge linalotokana na watu wasio wanasiasa wengi kama ilivyokua Bunge lililotunga Katiba Inayopendekezwa.

### 3.2.2. Mapungufu ya Njia hii;

Mapungufu makubwa ya njia hii endapo itakubalika ni matumizi ya rasilimali fedha nyingi na muda mrefu kutumika. Hii ni kutokana na uhitaji wa kuitisha mikutano mingi na wadau mbalimbali kinyume na matakwa ya wengi wanaotaka mchakato wa katiba umalizike kwa haraka ili Katiba Mpya iweze kutumika katika chaguzi zilizopo karibuni.

Uhitaji huu wa Mabadiliko ya Katiba kukidhi mazingira yenye usawa katika uchaguzi ulijitokeza pia katika makubaliano kati ya Rais wa awamu ya Nne wa Tanzania Dk. Jakaya Mrisho Kikwete na Kituo cha Demokrasia (TCD) ambacho kinajumuisha vyama vyote vya siasa mnamo Septemba 2014.
Katika mkutano huo masuala ambayo walikubaliana ni kufanya mabadiliko muhimu manne katika Katiba ya Mwaka 1977 kabla ya uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2015, masuala hayo ni; (1) Haki ya Kuhoji Matokeo ya Urais Mahakamani, (2) Mshindi wa kiti cha Urais kupata asilimia zaidi ya 50 ya kura zote, (3) Kuundwa kwa Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi, na (4) Kuruhusiwa kwa Mgombea Huru. Mabadiliko haya nyeti yanaweza pia kufikiriwa kufanyika kabla ya uchaguzi wa Seriakli za Mitaa wa mwaka 2019 na Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020 ili kuleta mazingira ya uchaguzi yenye usawa, huru na kukubalika na wadau wa uchaguzi.

## 3.3. Kuundwa kwa Kamati ya Wataalam wa Katiba;

Njia nyingine inayopendekezwa ni kuundwa kwa Kamati ya Wataalam ya masuala ya Katiba na sheria ambayo itapewa Hadidu za Rejea zinazowaelekeza kuandaa Rasimu ya Katiba yenye kuoanisha maoni ya wananchi yaliyopo kwenye Rasimu ya Pili ya Katiba ya 'Tume ya Warioba' kwa upande mmoja na Katiba Inayopendekezwa kwa upande mwingine.

Kama ilivyoelezwa awali, mkwamo wa mchakato wa Katiba ulitanguliwa na kufanyika kwa kazi kubwa ya kuundwa kwa sheria za mchakato wa katiba, ukusanyaji wa maoni na Bunge Maalum la Katiba.

Hivyo endapo Timu ya Wataalam itaundwa itakua ni njia nyepesi na yenye tija kwa kujikita kuainisha maoni ya wananchi ambayo yalipatikana kwa njia shirikishi ya wananchi na vyombo mbalimbali vya kikatiba na Kisheria.

Njia hii pia imeweza kutumika na kusaidia kukwamua mkwamo wa mchakato wa katiba katika nchi mbalimbali ikiwemo nchi jirani ya Kenya kufuatia mkwamo wa mchakato wa kuandika Katiba Mpya na kupelekea vurugu na mauaji ya watu wasiopungua 1,500 baada ya uchaguzi mkuu wa Disemba 2007.

Ni dhahiri kwamba mchakato wa Katiba huambatana na muafaka wa kitaifa na uponyaji wa magonjwa makubwa yanayochochea mgawanyiko wa jamii katika masuala mbalimbali ya kitaifa kama Migogoro ya ardhi, Uwazi na Uwajibikaji katika uongozi, Utawala wa Sheria, Rushwa, Ufisadi, Kupungua umoja wa Kitaifa na Mamlaka ya Wananchi dhidi ya Serikali.

Endapo njia hii itaasiliwa kufufua mchakato, Tanzania ina mengi ya kujifunza kutoka katika nchi jirani ya Kenya ambapo Kamati ya Uwiano na Utangamano wa Kitaifa (KNDR) iliundwa mwaka 2008 kufuatia machafuko ya uchaguzi wa mwaka 2007.
Kamati hii pamoja na masuala mengine ilisimamia utekelezaji wa maboresho ya umoja wa kitaifa ikiwemo mabadiliko ya Katiba. Moja ya zao la Kamati hii ni kupelekea kuundwa kwa Kamati ya Wataalam ya Mabadiliko ya Katiba iliyokuwa na wajumbe 9 ikiongozwa na Bwana Nzamba Kitonga kama Mwenyekiti wa Kamati.

Kwa mujibu wa Sheria ya Mabadiliko ya Katiba ya Kenya ya Mwaka 2008 kazi ya Kamati ya Katiba ya Wataalam ilikuwa ni kuoanisha Rasimu Mbili za Katiba ambazo zilileta mvutano wa kijamii. Kutokana na Kamati hii, Katiba Mpya ya Kenya ya Mwaka 2010 ilipatikana kufuatia Kura ya Maoni ya Wananchi juu ya Katiba Inayopendekezwa iliyoandaliwa na Kamati ya Wataalam. Kura ya Maoni ilifanyika tarahe 4 Agosti 2010 na hatimaye kuzinduliwa kwa Katiba Mpya ya Kenya tarehe 27 Agosti 2010.

### 3.3.1. Faida za Kuunda Kamati ya Wataalam;

Faida ya kwanza ya kutumia Kamati ya Wataalam ni uwezekano wa kutumia uzoefu wa nchi jirani zaidi ya Kenya ambayo tunashabihiana kwa kiasi fulani mazingira ya kisiasa, kijamii na hata muktadha wa mkwamo wa mchakato wa katiba ambao ulidumu kwa zaidi ya miaka 5.

Pia kutokana na uwepo wa Rasimu ya Pili ya Katiba na Katiba Inayopendekezwa huku zikionekana kuwa na ushindani wa maudhui kutokana na mapungufu ya kimuafaka yaliyojitokeza katika ngazi ya Bunge Maalum la Katiba, kuundwa kwa Kamati ya Wataalam kutarahisisha kazi ya kuoanisha maoni ya Rasimu zote mbili na kupelekea kupatikana kwa Katiba Inayopendekezwa na wataalam ndani ya muda mfupi na kwa kutumia gharama ndogo zaidi.

### 3.3.2. Mapungufu ya Kuunda Kamati ya Wataalam;

Mapungufu makubwa ya njia hii endapo itatumika ni utayari wa makundi mbalimbali ya wadau wa mchakato kutokua na utayari wa kushiriki kikamilifu kwa kutoaminiana na kuwa na imani ndogo juu ya nia ya serikali na vyombo vitakavyotakiwa kuratibu mchakato. Msingi wa hofu hii unajengwa na namna ambavyo mkwamo wa mchakato ulijitokeza kwa kuambatana na mgawanyiko mkubwa wa jamii haswa katika ngazi ya Bunge Maalum la Katiba na hatimaye hali hiyo kufifisha umoja wa kitaifa. Hivyo, itahitajika kuwepo kwa mjadala wa wazi wa makundi ya kijamii ikiwemo vyama vya siasa kujenga muafaka wa kitaifa na ushawishi mkubwa juu ya nia njema ya kuendeleza mchakato wa Katiba kupitia Kamati ya Wataalam.

## HITIMISHO

Mchakato wa Mabadiliko ya Katiba ambao umeshirikisha wananchi kwa kiasi kikubwa kama ilivyokuwa nchini Tanzania kupitia Tume ya Mabadiliko ya Katiba huweza kuchangia mabadiliko makubwa ya kitaifa katika nyanja mbalimbali ikiwemo masuala ya Uchumi, Siasa na jamii kwa ujumla. Mchakato unapokwama pasipo muafaka wa kitaifa huweza kuzalisha mazingira ya kufifia kabisa kwa umoja wa kitaifa na hatimaye kudumaza maendeleo ya nchi.

Madhara makubwa ya kukosekana kwa muafaka wa kitaifa hatimaye huweza kijiakisi kwa kiasi kikubwa kupitia masuala nyeti ya kikatiba ikiwemo chaguzi za Serikali za Mitaa na Uchaguzi Mkuu wa Rais, Wabunge na Madiwani na kusababisha mazingira hatarishi kwa amani na umoja wa Kitaifa. Hivyo ni muhimu sana kutafuta ufumbuzi wa mkwamo wa mchakato wa mabadiliko ya katiba kuepuka uwezekano wa mgawanyiko mkubwa zaidi wa kitaifa kama ilivyojitokeza kwa nchi nyingine ikiwemo nchi jirani ya Kenya na hivyo kudumaza juhudi kubwa za maendeleo ya taifa la Tanzania.

**Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu**
Jengo la Justice Lugakingira, Kijitonyama
S. L. P. 75254, Dar es Salaam – Tanzania
**Simu:** +255 22 2773038/48; **Nukushi:** +255 22 2773037
**Barua Pepe:** lhrc@humanrights.or.tz
**Tovuti:** www.humanrights.or.tz
**Kanzidata:** katiba.humanrights.or.tz

**Ofisi ya Arusha**
Mtaa wa Olerian, Kiwanja Na.116/5, Sakina kwa Idd
S. L. P 15243, Arusha Tanzania,
**Simu:** +255 27 2544187
**Barua pepe:** lhrcarusha@humanrights.or.tz

**Kituo cha Msaada wa Sheria**
Mtaa wa Isere- Kinondoni
S. L. P. 79633, Dar es Salaam – Tanzania
**Simu/ Nukushi:** +255 22 27612015/6
**Barua Pepe:** legalaid@humanrights.or.tz

@humanrightstz LHRC Tanzania